

SISI NI DOL YAKO



Department
of Labor

DIVISHENI YA SERA NA MAMBO YA WAHAMIAJI

DIVISHENI YA SERA NA MAMBO YA WAHAMIAJI (DIPA)

DIPA uhakikisha kwamba huduma, mipango, na ulinzi wa Idara ya Kazi unapatikana kwa wafanyakazi wote. Hii inajumuisha makundi yanayokua ya watu waliohamia Jimbo la New York kutoka nchi nyingine na wale ambao wanaongea lugha nyingine kando na Kiingereza.

JITIHADA

DIPA huwafahamisha wahamiaji, wakimbizi, na Wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiingereza (ELL) kuhusu haki za mahali pa kazi. Tunawaelezea kuhusu msaada unaotolewa na DOL, kama vile:

- Hatua kuhusu mishahara isioliipwa, muda wa ziada, na faida nyingine
- Maelezo kuhusu bima ya kutoajiriwa
- Msaada wa kutafuta kazi na msaada wa kazi
- Viungo vya mashirika mengine na makundi yanayoweza kusaidia
- Maelezo kuhusu biashara haramu ya Usafirishaji wa Wanadamu

DIPA pia huwaelimisha wamiliki wa biashara ndogo kuhusu:

- Sheria za ajira
- Majukumu yao ya kisheria
- Rasilimali za DOL ambazo zinaweza kuwasaidia
- Biashara haramu ya Usafirishaji wa Wanadamu

SERA NA SHERIA

DIPA hufanya kazi ili kuhakikisha kwamba Idara ya Kazi ya Jimbo la New York inatimiza mahitaji ya wahamiaji, wakimbizi na Wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiingereza. Sisi hupitia jinsi sera za NYSDOL, taratibu na sheria zinavyoathiri jamii zao.

WAHADHIRIWA WA UHALIFU

Biashara haramu ya Usafirishaji wa Wanadamu na kazi ya kushurutishwa ni uhalifu ambao huwatumia vibaya wakazi wa New York, ikiwa ni pamoja na wahamiaji, wakimbizi na Wanafunzi Wanaojifunza lugha ya Kiingereza. DIPA husaidia kukabiliana na tatizo hili katika jimbo lote. Tunawaelekeza pia wahadhiriwa kwa mashirika ya serikali ambayo yanaweza kuwasaidia kupata huduma wanazostahili chini ya sheria za uhalifu za jimbo.

Wahadhiriwa wa uhalifu huu wanaweza kuomba serikali kuu visa maalum. Ili kuomba, lazima wathibitishwe kupitia shirika la utekelezaji sheria. Katika DOL, DIPA hupitia maombi ya uthibitishaji wa visa ya U na T.

KILIMO

DIPA hufanya kazi ili kuimarisha tasnia kubwa na pana ya kilimo ya New York. Kwa wakati huo, tunawafunza wafanyakazi wa kilimo kuhusu haki zao na huduma zinazopatikana kupitia DOL. Tunatembelea mashamba ili kuwasaidia wafanyakazi kutii sheria za kazi. Tunawasaidia pia wakulima kupata wafanyakazi wa kilimo waliohitimu ili kutumiza mahitaji yao ya kikazi. DIPA huchakata maombi ya H-2A, hutekeleza ukaguzi wa majengo, hutoa msaada wa mahojiano ya lugha ya Kihispania, na hufanya kazi ili kusaidia Idara ya Kazi ya Marekani katika kuhakikisha kwamba mikataba ya H-2A imeafikiwa.

WASILIANA NA DIPA

Simu: **877-466-9757 (877- IMM-WRKR)**

Barua-pepe: **dipa@labor.ny.gov**

Tovuti: **www.labor.ny.gov**